BUKU LA 14
Salamu kwa familia ya Wilaya ya Shule za Jimbo la DeKalb

Ninatumaini kwamba ulikuwa na juma njema. Asante kwa kila mtu kwa maoni yao tunapokuwa tukijiandaa kurudi kwa masomo ya ana kwa ana. Wilaya inafuatilia mwongozo kutoka kwa Idara ya Afya ya Umma ya Georgia (DPH), Idara ya Elimu ya Georgia, na Halmshauri ya Afya ya Kaunti ya DeKalb. Kama matokeo ya data ya mtindo kutoka kwa Halmshauri ya Afya ya Kaunti ya DeKalb ya wastani wa siku 14 kwa wakazi 100,000 wa Kaunti ya DeKalb, tunaandaa kuhamisha wilaya kwa Awamu ya II ya mpango wetu wa ana kwa ana ikiwezekana. (Kanusho: Idara ya Afya ya Umma ya Georgia huripoti idadi na kusasisha data huku maelezo mapya yakipatikana).

Hadi leo, wastani ni 103. Wastani huu utaendelea kufuatiliwa kila siku kwa sababu tumechagua kuongozwa na sayansi na data inayopatikana. Jopokazi la COVID-19 la Kufungua Upya Shule la DCSD linaendelea kufuatilia mitindo na kufanya marekebisho kama yanavyohitajika ili kuhakikisha usalama na ustawi wa wanafunzi, kitivo, na wafanyakazi wote.

Tangu mara ya mwisho kuwasiliana, tumekutana na Makundi ya Kuwashauri Wazazi na Waalimu ya DCSD na walimu wengi wakuu ili kupokea maoni yao. Wilaya inafahamu kuhusu wazazi na washikadau wa jamii walio na wasiwasi ambao wameshiriki maoni yao tofauti kuhusu kurudi kwa masomo ya ana kwa ana. Ijapokuwa tunatambua kwamba kuna wazazi wanaotamani kufunguliwa kwa shule mara moja, ni muhimu kukumbuka kwamba ni lazima tusawazishe wasiwasi wa washikadau wote wa jamii ili kufungua tena shule kwa usalama kupitia njia ya awamu.

Wataalamu wa COVID-19 wa DCSD hukutana kila siku na wataendelea kutathmini kinachohitajika ili kuhakikisha kwamba madarasa yetu, vituo, na mabasi ni salama, na kwamba tuna mazingira salama kwa washikadau wote wa DCSD. Kulinda usalama wa wanafunzi, waalimu na wafanyakazi wetu wakati wa janga hili linaloendelea kunasalia kuwa kipaumbele cha kwanza cha Wilaya.

Wafanyakazi
Mnamo Oktoba 19, Jopokazi la COVID-19 la Kufungua Tena Shule la DSCD litawasilisha mpango uliosasishwa kwa Halmashauri ya Elimu ya Kaunti ya DeKalb kuhusu muda wetu. Tunaendelea kuboresha Mpango wetu wa Masomo ya Ana kwa Ana kulingana na maoni kutoka kwa wazazi, waalimu, na washikadau wengine wa jamii.

Wanafunzi
Kama ilivyojadiliwa katika sasisho la wiki iliyopita, wanafunzi wanaendelea na mazingira ya masomo ya mbali katika Awamu ya II kabla ya kuhamia Awamu ya III. Katika Awamu ya III, wazazi/walezi wana chaguo la masomo mseto au masomo ya mbali. Fomu ya Kubadilisha Nia ya Kurudi Shule ilisambazwa mnamo Octoba 9 ili

wazazi/walezi waweze kuchagua chaguo lao wanalopendelea kwa kila mtoto. Majibu haya yataruhusu shule za nchini kuwapanga wanafunzi kwa makundi madogo ili kudumisha mahitaji ya kutokaribiana darasani wakati wa masomo mseto na kupanga wanafunzi ambao wataendelea kusoma mtandaoni nyumbani wakati Awamu ya III itaanza.

Kiungo: https://dekalb.co1.qualtrics.com/jfe/form/SV_cO7CQFP10BWfwuF

Miundo ya masomo ya kuzingatia ni kama yafuatayo:

Muundo wa Masomo Mseto (Mchanganyiko wa Masomo ya Ana kwa Ana na ya Mbali):

Muundo wa masomo mseto umeundiwa familia zinazohisi sawa kuwarudisha watoto wao kwa mazingira ya masomo ya ana kwa ana yaliyochanganywa na masomo ya mbali. Wanafunzi watakuwa na nafasi ya kutangamana na waalimu na wanafunzi wenza kwa usalama. Familia zinaweza kuchagua muundo wa masomo ya mbali wakati wowote ule kwa kukamilisha Fomu ya Kubadilisha Nia ya Kurudi Shule katika shule ya ndani.

Wanafunzi na wafanyakazi watahitajika kuvaa vifunika uso au barakoa. Pia, wanafunzi watahitajika kuleta shuleni vifaa vyao vya elektroniki walivyopewa na wilaya au vya kibinafsi.

Muundo wa Masomo ya Mbali:

Muundo wa masomo ya mbali umeundiwa familia ambazo hazihisi vizuri watoto wao wakirudi shuleni katika mazingira ya ana kwa ana kwa wakati huu. Wanafunzi wataendelea kusoma kutoka nyumbani katika mazingira ya mtandaoni yanayotolewa na shule. Familia zitakuwa na nafasi ya kubadilisha kwa muundo wa sasa wa masomo ya ana kwa ana katika kipindi cha kila wiki 4.5 na kukamilisha Fomu ya Kubadilisha Nia ya Kurudi Shule katika shule ya ndani.

Familia zote zinahimizwa kukamilisha Fomu ya Kubadilisha Nia ya Kurudi Shule kabla ya Oktoba 23, 2020. Kabla ya kukamilisha fomu, tafadhali pata nambari ya utambulisho wa mwanafunzi wako (nambari ya chakula cha mchana au nambari ya kuingia ya Chromebook). Ikiwa huna nambari ya utambulisho ya mwanafunzi wako, tembelea Kituo cha Wazazi, angalia ripoti ya hivi karibuni ya maendeleo ya mtoto wako, au wasiliana na mwalimu wa mtoto wako.

Kuwaandaa wanafunzi wetu na familia zao kwa awamu ifuatayo ya mpango wetu wa kufungua tena shule ndio kipaumbele chetu. Unaweza kuendelea kutarajia taarifa za mara kwa mara kuhusu mpango wa kufungua tena kupitia jarida hili, ukurasa wetu wa wavuti wa DCSD, tovuti za shule, messenger ya shule na mitandao ya kijamii (Facebook, Twitter, na Instagram).

Uwanjani

Nilikuwa na fursa ya kujiunga na Msimamizi wa Eneo la I, Bi. Melanie Pearch kwa ziara ya nje. Msimamizi wa Mkoa Pearch na mimi tulitembelea Shule ya Msingi ya Ashford Park, Shule ya Msingi ya Doraville United, na Shule ya Upili ya Chamblee. Hongera kwa Kittredge Magnet ES na Austin ES kwa kuwa Shule za Blue Ribbon. Ilikuwa vizuri pia kuona kwamba Cross Keys imepata wanafunzi wengi na waalimu wakuu wakongwe katika kundi hili ambao wamejitolea kwa shule zao. Kwa alivyosema Mwalimu Mkuu, Cedric Anthony, Shule ya Kati ya Sequoyah, “Tunapanda mbegu ya kusaidia miti kukua ambayo inatoa kivuli ambacho hatutawahi kuwa chini yake.”

Asante kwa familia nyingi ambazo zinaendelea kuchukua muda wa kuwasiliana na mimi na kuuliza maswali au kushiriki maoni yao ya thamani. Katika juhudi za kuhakikisha kwamba kila mtu anapokea majibu, tafadhali elekeza maswali na maoni yako kwa msimamizi na waalimu wako wakuu wa mkoa. Ninajua kwamba huu ni wakati wenye dhiki sana kwa familia zetu nyingi za DCSD. Tunapokuwa tukipitia mwaka wetu wa shule unaobadilika, ninataka kusisitiza ahadi yangu imara kwa usalama wa wanafunzi wetu na ufanisi wa kielimu.

Shabiki wako wa #1,

Cheryl Watson-Harris